



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*



www.nishati.go.tz



Wizara ya Nishati



wizara_ya_nishati_tanzania



@Nishati2017



Wizara ya Nishati

Toleo Namba 15

Juni 1-30, 2020

WAZIRI KALEMANI AKUTANA NA WAKANDARASI WA REA KUJADILI UMEME VIJIJINI

»» Apongeza utendaji kazi wa REA, TANESCO na Wakandarasi

»» Asema REA imetengeneza historia Tanzania

»» Muda wa kukamilisha miradi haujabadilika



UK.
2

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (mstari wa mbele), wakishiriki kikao cha Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kulia) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

NAIBU WAZIRI NISHATI AZINDUA MRADI WA UMEME JUA NANJIRINJI

UK.
6



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), alipokutana nao jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo Mradi huo.

WAZIRI KALEMANI AKUTANA NA WAKANDARASI WA REA KUJADILI UMEME VIJIJINI

**Veronica Simba na
Zuena Msuya – Dodoma**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amekutana na wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza na kujadiliana maendeleo ya mradi huo unaotekelzewa nchini kote.

Kikao hicho kilichofanyika Mei 21, 2020 jijini Dodoma kilihudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgali, Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini

(REA), Wakili Julius Kalolo pamoja na Wajumbe wa Bodi hiyo.

Wengine ni Kaimu Kamishna wa Nishati Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt. Tito Mwinuka, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA Mhandisi Amos Maganga na Menejimenti yake, Mameneja wa TANESCO wa Kanda pamoja na Wasimamizi wa Mradi husika kutoka Wizarani.

Akifungua kikao husika, Dkt. Kalemani aliwapongeza Wakandarasi hao kutokana na kazi wanayoifanya ya kusambaza umeme

vijijini lakini akabainisha msimamo wa Wizara kuwa haitarajji kuongeza muda wa kukamilisha kazi husika, hivyo akawataka kuongeza bidii na ubunifu ili waweze kukamilisha kazi ifikapo Juni 30, mwaka huu kama ilivyoinishwa katika Mkataba.

"Pamoja na kwamba wengi wenu mnafanya kazi nzuri lakini wapo wachache ambao wanasuasua. Ninawataka mjipime kutokana na utendaji wenu kama mtastahili kuendelea na kazi nydingine zitakazofuata," aliasa Waziri.

Akifafanua zaidi, alisema Wizara kamwe haitaingia mikataba mipya ya kazi na wakandarasi wababaishaji huku

akisisitiza kuwa ni wale tu wanaofanya vizuri katika miradi ya sasa ndiyo watakuwa na nafasi ya kupewa kazi nydingine.

Katika hatua nydingine, Waziri aliwataka wakandarasi hao kutambua kuwa wao ni watumishi wa umma hivyo akawataka kufanya kazi kwa weledi na uzalendo huku wakizingatia maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwani ndivyo watumishi wa umma wanavyopaswa kuwa.

Alifafanua kuwa, mtumishi wa umma ni ye yeyote aliyeajiriwa au kuingia mkataba na Serikali kufanya kazi fulani na ataendelea kuwa na sifa

Mwanakijiji swala la nguzo halikuhusu!lipia upate umeme



BODI YA UHARIRI

Mhariri

Veronica Simba

(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

Waandishi

Veronica Simba

Teresia Mhagama

Zuena Msuya

Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148 au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P.
2494, 40474 Dodoma

www.nishati.go.tz

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara_ya_nishati_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)

Kwenu wasomaji na wadau wetu wa sekta ya nishati, leo tunazungumzia baadhi ya wanakijiji kuacha kulipia gharama za kunganishiwa umeme wakisubiri nguzo kufika katika maeneo yao, hali ya kuwa tayari umeme ushafika katika kijiji husika.

Ndugu zangu hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya vijiji 9,112, kati ya 12,268 Tanzania nzima vimeunganishiwa umeme, lengo ni kuhakikisha kuwa kila mtanzania anatumia nishati ya umeme katika makazi yake hivyo ifikapo mwezi Juni 31, 2021 vijiji vyote Tanzania vitakuwa vimeunganishiwa na umeme.

Ili kutekeleza azma hiyo ya serikali, Waziri mwenye dhamana ya kusimamia sekta ya nishati, Dkt. Medard Kalemani amewaambia wakazi wa vijiji ambavyo umeme umeshafika katika maeneo yenu mlipio gharama za kuwashishiwa umeme ili kufahamu idadi ya wateja, nguzo zisambazwe na kuunganishiwa kulingana na wateja waliopo kwa wakati husika.

Dkt. Kalemani alisema kuwa kuna dhana imejengeka kwa baadhi ya wanavijiji kuwa hawalipii gharama wala kusuka nyaya katika nyumba zao, hadi pale watakaponia nguzo zimesambaa katika maeneo yao, jambo ambalo si sahihi, ni vyema sasa kila mwanakijiji ambaye katika eneo lake umeme umefika basi alipie gharama ili nguzo zije na awashiwe umeme.

Kwa kufanya hivyo kutarahishisha kazi ya kuwafikia wateja kwa haraka na kuwashishiwa umeme kwa wakati, kwa kuwa tayari vijiji vingi vimefikiwa na umeme katika maeneo machache na kazi

kubwa iliyopo ni kuusambaza tu kwa watumiaji hivyo wananchi wanatakiwa kulipia gharama waunganishiwe wasisubiri nguzo.

Alikaririwa akiwaeleza wanakijiji hao kuwa hawapaswi kuhoji kuhusu nguzo kufika katika maeneo yao kwakuwa hilo si jukumu lao, ila wanachotakiwa kufanya ni kulipia gharama za kuwashishiwa umeme tu, na baada ya kulipia gharama ndipo wahoji endapo hawajawashiwa umeme.

"Kijiji chochote ambacho umeme umeshafika na kuunganishiwa, hata kama umewashishiwa katika nyumba moja, wanakijiji sasa jukumu lenu ni kulipia gharama kuwashishiwa umeme ili ijulikane idadi ya wateja waliopo na mletewe nguzo na kuungwa, nguzo zinaletwa na kusambazwa kulingana na idadi ya wateja waliopo, kwa wakati husika ili wote wanaotaka kwa wakati huo wapate, msihoji kuwa nguzo zinifikia lini hilo si jukumu lenu! Ninyi mnapaswa kuhoji lini mtawashishiwa umeme mkiwa tayari mmelipia gharama, na hapo tutachukua hatua kwa ye yote atakayechelewa kumuwashishiwa umeme mteja aliyekwisha lipia gharama za uunganishi, Sasa lipieri misisubiri nguzo", Alisema Dkt. Kalemani

Pia alieleza kuwa kitendo cha wanakijiji kuacha kulipia gharama za kuwashishiwa umeme wakisubiri kuona nguzo kusambaa katika maeneo yao, hali ya kuwa tayari umeme umeshafika katika vijiji vyao, kunachelewesa kasi ya kuwashishiwa umeme wanakijiji katika nyumba zao, hivyo wananchi wachangamkie fursa na kulipia gharama ya shilingi 27,000 tu wapate umeme.

Katunika Ki-nishati



WAZIRI KALEMANI AKUTANA NA WAKANDARASI WA REA KUJADILI UMEME VIJIJINI

INATOKA UK.

2

hiyo hadi pale mkatuba wake unapokoma.

Aidha, Waziri alitoa pongezi za pekee kwa wakandarasi ambao hadi sasa wamekamilisha kazi kwa asilimia nyngi huku wakiwa na uelekeo wa kukamilisha kazi husika muda mfupi kutoka hivi sasa.

Wakandarasi hao walitajwa kuwa ni Kampuni za Steg International Ltd anayetekeleza Mradi katika mikoa ya Mbeya na Songwe, Sengerema Engineering Group Ltd (Iringa), Derm Electrics (T) Ltd (Tanga) na Nakuroi Investment Co. Ltd (Rukwa).

Vilevile, Waziri alitoa pongezi kwa Bodi ya Wakurugenzi wa REA kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia miradi husika. Pia, aliipongeza Menejimenti ya Wakala huo na watumishi wake wote huku akiipambanua Taasisi hiyo kwamba

imetengeneza historia Tanzania.

"Tanzania sasa inasifika kwa kazi nzuri ya usambazaji umeme vijijini. Hilo limewezezana kwa uchapakazi wenu. Hongereni sana."

Sambamba na REA, Waziri pia aliipongeza TANESCO, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa utendaji wao mahiri ambao alieleza umewezesha mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika kikao hicho, Naibu Waziri Mgali na Katibu Mkuu Mhandisi Said, pamoja na kuunga mkono pongezi alizotoa Waziri kwa REA, TANESCO na Wakandarasi, pia walitoa nasaha kwao.

Naibu Waziri alisema, miradi ya REA ili itekelezwe kwa ufanisi, inahitaji ushirikiano baina ya pande zote ambazo ni mwajiri, mwajiriwa na wadau wote wanaohusika.

"Serikali tunathamini na tunaahidi kuendelea kuwajengea mazingira



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgali akizungumza na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatoo, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani) wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi hao kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

mazuri ili muweze kukamilisha kazi zenu kwa wakati na viwango."

Naye Katibu Mkuu aliwaasa wakandarasi kujenga mahusiano mazuri na viongozi pamoja na wananchi wote katika maeneo wanakotekeliza miradi, ili iwasadie kupata ushirikiano katika utekelezaji wa kazi zao.

"Unapoaminiwa, basi jitahidi ili nawe ufanye

ile kazi kwa kiwango kinachostahili ili uendelee kuaminiwa," alisitiza Katibu Mkuu.

Wizara ya Nishati imejijengea utamaduni wa kufanya mikutano ya aina hii mara kwa mara ili kutoa fursa ya majadiliano baina ya pande zote, kwa lengo la kuboresha utendaji kazi kwa manufaa ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (wa pili kushoto) akizungumza na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatoo, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi hao kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgali na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini REA, Wakili Julius Kalolo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakili Julius Kalolo, wakisikiliza maoni ya Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatoo, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani) wakati wa kikao katika yao na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani), kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

MATUKIO PICHANI



Kutoka kulia ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga na Mkurugenzi wa Huduma za Ufundu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Jones Olotu, wakifuatilia kikao kati cha Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (mstari wa mbele), wakishiriki kikao cha Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgali (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Amos Maganga, wakifuatilia kikao cha Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgali (kushoto) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kulia) wakifurahia jambo wakati wakitoka katika Ukumbi kulipofanyika kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, kujadili maendeleo ya Mradi huo. Kikao kilifanyika jijini Dodoma Mei 21, 2020.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka akizungumza na wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi hao kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Amos Maganga akizungumza na wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (hawapo pichani), wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na Wakandarasi hao kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.



Mmoja wa wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza, Mhandisi Bengiel Msufe, akitoa maoni wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) na wakandarasi hao kilichofanyika jijini Dodoma, Mei 21, 2020 kujadili maendeleo ya Mradi huo.

NAIBU WAZIRI NISHATI AZINDUA MRADI WA UMEME JUA NANJIRINJI



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (kushoto) akisisitiza jambo, mara baada ya kuzindua rasmi mradi wa umeme jua Nanjirinji, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi, Mei 17, 2020. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai.

Na Veronica Simba –
Lindi

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo amezindua rasmi mradi wa umeme jua unaotekelizwa katika vijiji vya Kata ya Nanjirinji, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi.

Akizungumza na viongozi wa eneo lai hilo akiwemo Mkuu wa Wilaya, Diwani na viongozi wa vijiji husika, muda mfupi kabla ya kufanya uzinduzi, Mei 17, 2020, Naibu Waziri alieleza kuwa mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya umeme wananchi wakati serikali ikijiandaa kupeleka umeme wa uhakika kupitia mradi wa umeme vijijini.

"Tunashukuru Bunge kwa kupitisha bajeti ya Wizara yetu kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambayo pamoja na mambo mengine, imejikita katika upelekaji umeme vijijini. Nafurahi kuwajulisha kuwa vijiji vya Nanjirinji ni mionganoni mwa

vitakavyopelekewa umeme ndani ya kipindi husika," alisema.

Aidha, Naibu Waziri alieleza kuwa mradi huo ambao pia unatekelezwa Kilwa kisiwani ni mpango mkakati wa Serikali kuhakikisha wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo mbali na miundombinu ya umeme mkubwa, vikiwemo visiwa, wanafikishiwa pia huduma ya umeme ili waweze kunufaika sawa na wananchi wa maeneo mengine.

Aliwataka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambao ndiyo wafadhili wa miradi ya aina hiyo kote nchini, kujenga utaratibu wa kutembelea miradi hiyo ili kujiridhisha endapo fedha zilizotolewa na Wadau wa Maendeleo katika kutekeleza miradi hiyo zinatumika kwa tija.

Kwa mantiki hiyo, aliwataka Wakala huo kuanzisha kitengo cha tathmini na ufuatiliaji, ambacho kitashughulikia

masuala hayo katika miradi yote ya umeme jadidifu.

Halikadhalika, alitoa maelekezo hayo kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

"TANESCO ninyi ndiyo mnahusika na uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, hivyo mnawajibika pia kufuatilia miradi hii na kufanya tathmini badala ya kuwaacha wananchi wakiwa hawana pa kukimbilia kueleza changamoto wanazokabiliana nazo."

Alisema, katika ziara zake sehemu mbalimbali nchini kukagua miradi ya aina hiyo, amekuwa akipokea malalamiko ya wananchi kuwa miradi hiyo haina mfuatiliaji badala yake anaachwa mkandarasi pekee pasipo usimamizi.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri alitumia fursa hiyo kuwaeleza viongozi hao kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imeanza kulipa fidia kwa wananchi

wa eneo la Likong'o mkoani humo, ambao wamepisha mradi wa kuchakata gesi.

Alisema jumla ya shilingi bilioni tano zimetolewa na kwamba mazungumzo yanaendelea baina ya serikali na wawekezaji kuhusu kuanza kwa ujenzi wa kiwanda hicho kitakachochochaea uchumi wa Mkoa wa Lindi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya viongozi walioshiriki tukio hilo, waliipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuwapelekea huduma hiyo ya umeme lakini wakaomba wapelekewe umeme wa uhakika zaidi kulingana na mahitaji makubwa waliyonayo hususani katika kuendesha viwanda vya kuchakata ufuta ambao huzalishwa kwa wingi wilayani humo.

Aidha, walimwomba Naibu Waziri aflikishe kilio chao cha ubovu wa barabara kwa Waziri mwenye dhamana ya miundombinu, wakisema hiyo ni changamoto kuu katika eneo hilo.

Mradi huo wa Umeme Jua ulianza kutekelezwa mwaka 2017 na ulipangwa kukamilika mwaka huu wa 2020. Mradi umelenga kuunganisha umeme kwa wateja 80 katika vijiji vya Nanjirinji, ambao hata hivyo imeelezwa kuwa mahitaji yameongezeka kufikia wateja 350 wenye uhitaji.

Gharama ya mradi ni Dola za Marekani 40,000 ambapo mpaka sasa, Mkandarasi (Kampuni ya Greenleaf Technology Solutions Limited) amekwahilipwa asilimia 70 ya gharama hizo, ambazo ni Dola za Marekani 28,000.

MAWAZIRI KALEMANI NA ZUNGU WAKAGUA MABWAWA YA KIDATU NA MTERA



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (wa pili-kulia) Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Zungu (wa pili kutoka kushoto) na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said (wa kwanza-kulia) wakiwasili katika Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Mtera lililopo Iringa wakati wa ziara ya kukagua mabwawa hayo Mei 7, 2020.

Hafsa Omar - Morogoro

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani alisema Serikali imeunda timu ya wataalam itayoweka mipango kazi

ya kukabiliana na athari za mvua zilizojitokeza katika mabwawa ya kuzalisha umeme wa maji.

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani alisema hayo Mei 7, mwaka huu alipofanya ziara ya kikazi kwenye vituo vya



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (wa kwanza-kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Loata Ole Sanare (katikati) na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said (kulia) wakiwa kwenye ziara ya kazi kukagua Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Kidatu, mkoani Morogoro, Mei 7, 2020.

kufua umeme wa maji vya Mtera (Iringa) na Kidatu (Morogoro) akiwa ameambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Zungu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Dkt. Kalemani alisema lengo la ziara hiyo ni kuhakikisha kuwa maji kutosha yanapatikana kuzalisha umeme wa uhakika pamoja na kuangalia athari za mazingira kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Alisema, kufuatia athari zilizojitokeza katika kipindi cha mvua, Serikali imeunda timu ya wataalam itakayoongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said ambayo itapaswa kuandaa mipango kazi kwa ajili ya kukabiliana na athari zilizojitokeza katika mabwawa hayo.

Akielezea kuhusu uwezo wa Bwawa la Kidatu, Dkt. Kalemani alisema kuwa lina kima

cha ujazo wa mita 450 na ikitokea maji yakaja zaidi, hufunguliwa kuruhusu maji kutoka, na kwenda katika Bwawa la Rufiji, hivyo akawataka wataalamu wanaohusika na shughuli hiyo kuhakikisha kuwa maji wanayiyafungulia hayaleti madhara na athari yoyote kwa mazingira na jamii.

"Tuna jukumu kubwa la kuhakikisha maji hayaleti madhara. Nilipokuja awali, niliona madhara katika baadhi ya maeneo ndiyo maana nikaunda timu kupitia kwa Katibu Mkuu na baadhi ya viongozi wa mikoa inayozunguka bwawa hili ili wahakikishe maji hayaleti madhara kwa wananchi."

Vilevile, alitoa wito kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya mito kuchukua tahadhari ili wasiathirike katika kipindi



Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kukagua Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Kidatu lililoko mkoani Morogoro, Mei 7, 2020. Katikati ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Zungu.

MAWAZIRI KALEMANI NA ZUNGU WAKAGUA MABWAWA YA KIDATU NA MTERA

INATOKA UK.

7

cha mvua kubwa, na kuwataka kutunza vyanzo vya maji kwa kulima kwa ustarebu pasipo kuathiri vyanzo hivyo.

Pia, aliwataka wataalamu kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha kipindi ambacho kuna maji ya kutosha, umeme uzalishwe wa kutosha na kutouzima kwa sababu hakuna sababu ya kufanya hivyo.

Kwa upande wake, Waziri Zungu alisema lengo la Serikali ni kulinda vyanzo vya maji kwani yakikosekana, uzalishaji wa umeme nchini utashuka hali inayoweza kusababisha uchumi wa nchi kuyumba.

"Vyanzo hivi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mara baada ya Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (kulia), kukagua Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Kidatu lililoko mkoani Morogoro, Mei 7, 2020.

visipolindwa vitashindwa kusafirisha maji kwenda kwenye miradi mikubwa kama ule wa umeme wa

Julius Nyerere, hivyo ni lazima tuvilinde vyanzo vyetu kwa umakini zaidi," alisema.

Aidha, alitoa siku kumi kwa timu iliyoundwa, kutoa taarifa rasmi inayobainisha ni kwa namna gani vyanzo vya maji vitalindwa katika kuhakikisha kunakuwa na umeme wa uhakika nchini.

Naye Katibu Mkuu, Mhandisi Zena Said, alisema kuwa ye ye pamoja na timu yake, wataaka na wataalamu mbalimbali ili kuangalia data za miaka ya nyuma kusudi wa one namna nzuri ya kuzitumia kuweka mipango ya kuzuia uharibifu usitokee kwenye vyanzo hivyo vya umeme.

Aidha, viongozi wengine walioshiriki ziara hiyo pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Taasisi zilizochini yake pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said (kushoto) akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu (hawapo pichani), wakazi wa ziara ya kukagua Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Kidatu lililoko mkoani Morogoro, Mei 7, 2020.



Taswira ya Bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Kidatu lililoko mkoani Morogoro, Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Zungu, walifanya ziara ya kukagua mabwawa hayo Mei 7, 2020.


Dkt. Kalemani: Lipieni tujue idadi ya wateja tusambaze nguzo tuwawashie umeme!

Na Zuena Msuya Geita,

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amewaambia wanakijiji ambao umeme ushafika katika maeneo yao walipie garama za kuwashawa umeme ili kufahamu idadi ya wateja, nguzo zisambazwe na kuunganishwa kulingana na wateja waliopo kwa wakati husika.

Dkt. Kalemani alisema hayo wakati akiwasha umeme katika Kijiji cha Rusungwa Kata ya Nyamirembe, Bugwego Kata ya Bwongera Wilayani Chato na Kijiji cha Businda Wilayani Bukombe mkoani Geita alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika maeneo hayo, Mei 18, 2020.

Dkt. Kalemani alisema kuwa vijiji vingi tayari vimefikiwa na umeme katika maeneo



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) akiwasha umeme katika Kijiji cha Bugwego Kata ya Bwongera, wilayani Chato mkoani Geita alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika maeneo hayo, Mei 18, 2020.

machache hivyo wananchi wanatakiwa kulipia garama za kuwashawa umeme ili ifahamike idadi ya wateja waliopo na kupelekewa nguzo za kusambazwa kwa wateja waliopo na wawashiwe umeme.

Pia alieleza kuwa kitendo cha wanakijiji

kuacha kulipia garama za kuwashawa umeme wakisubiri kuona nguzo zimesambaa katika maeneo yao, hali ya kuwa tayari umeme umeshafika katika vijiji vyao, kunachelewesha kasi ya kuwashawa umeme wanakijiji katika nyumba zao kwa kuwa mamlaka



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto), akizungumza na mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Rusungwa Kata ya Nyamirembe, Wilayani Chato, mkoani Geita baada ya kuwashawa umeme katika nyumba yake alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika maeneo hayo, Mei 18, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (kushoto) akiruka maji wakati akienda kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini katika Kijiji cha Bugwego Kata ya Bwongera Wilayani Chato, mkoani Geita, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika maeneo hayo, Mei 18, 2020. Dkt. Kalemani alilazimika kutembea kwa mguu kufikia maeneo hayo kuwa magari hayafiki kwa sababu ya kuharibika kwa barabara kufuatia mvua kubwa zilizokuwa zinanyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

husika zinasambaza nguzo kulingana na wateja waliopo eneo husika kwa wakati husika, hivyo wananchi wachangamkie fursa na kulipia gharama ya shilingi 27,000 tu.

Vilevile alisema kuwa wanakijiji hao hawapaswi kuhoji kuhusu nguzo kufika katika maeneo yao kwakuwa hilo si jukumu lao, ila wanachotakiwa kufanya ni kulipia gharama za kuwashawa umeme tu, na baada ya kulipia gharama ndipo wahoji endapo hawajawashiwa umeme.

"Kijiji chochote ambacho umeme umeshafika na kuunganishwa, hata kama umewashwa katika nyumba moja, wanakijiji sasa jukumu lenu ni kulipia gharama kuwashawa umeme ili ijulikane idadi ya wateja waliopo na mletewe nguzo na kuungwa, nguzo zinaletwa na kusambazwa kulingana na idadi ya wateja waliopo, kwa wakati husika ili wote wanaotaka kwa wakati huo wapate, msihoji kuwa nguzo zinafika lini hilo si jukumu lenu! Ninyi mnapaswa kuhoji lini mtawashiwa umeme mkiwa tayari

INAENDELEA UK.

10

Dkt. Kalemani: Lipieni tujue idadi ya wateja tusambaze nguzo tuwawashie umeme!

INATOKA UK.

9

mmelipia gharama, na hapo tutachukua hatua kwa yeyote atakayechelewa kumuwashia umeme mteja aliyekwisha lipia gharama za uunganishaji, Sasa lipieni msisubiri nguzo", Alisema Dkt. Kalemani

Aidha Dkt. Kalemani alirejea kusema kuwa mkandarasi yeyote atakayeshindwa kumaliza kazi ya usambazaji wa umeme vijiji kwa mujibu wa mkataba, atashitakiwa kisheria kwa kosa la kuwacheleweshea wananchi huduma pamoja na kukatwa asilimia 10 ya malipo yake yaliyosalia.

Aidha kazi hiyo atapewa mkandarasi mwengine amalizie na hiyo asilimia 10 iliyokatwa ndiyo itatumika kumlipa mkandarsi



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akiwasha umeme katika Kata ya Businda wilayani Bukombe mkoani Geita alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijiji katika maeneo hayo, Mei 18, 2020.

atakayekabidhiwa jukumu la kumalizia kazi hiyo.

Aliendelea kuwasitisiza wakandarasi walio nyuma ya muda katika kukamisha kazi hizo kuongea nguvu

kazi katika maeneo ya kazi ili wasikumbane na kadhia hivyo.

Vilevile alitoa wiki moja kwa mkandarasi kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania(



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) akizungumza na wakazi wa Kata ya Businda wilayani Bukombe mkoani Geita (hawapo pichani) alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijiji katika maeneo hayo, Mei 18, 2020.

TANESCO) kuwawashia umeme wakazi wa Mtaa wa Businda waliokwisha lipia gharama hizo na kukumuagiza Mkuu wa Wilaya ya Bukombe kumchukulia hatua mkandarasi wa eneo hilo endapo atashindwa kufanya hivyo.

Dkt. Kalemani alisema kuwa mkandarasi yeyote ambaye hakufanya vizuri katika utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme vijiji (REA), hatapewa nafasi ya kufanya kazi katika miradi inayokuja hata kama ameshinda vigezo vya Zabuni.

"Mkuu wa Wilaya nakukabidhi mkandarasi huyu akishindwa kuwauwashia umeme wanakijiji hao walolipia gharama pamoja na kuwaunganishia wale aliowapita pale, mchukulie hatua ikiwezekana muweke korokoroni, hii iwe fundisho kwa wakandarasi wengine nchini kwa sababu wengi wanachewa kuwawashia wananchi umeme wakati tayati wamelipia, na utaratibu ni ndani ya siku saba baada ya mwananchi kulipia awashiwe umeme sio kuwaacha tu bila kuwaeleza sababu yoyote", Alisisitiza Dkt. Kalemani.

Pia aliawawasisitiza mameneja wa TANESCO kote nchini kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza azma ya serikali ya kuunganisha umeme katika kijiji vyote nchini ifikapo 2021, pia wazingatie viwango na tathmini iliyowekwa katika kuwapima utendaji kazi wao.

Juni 30, 2020 wakandarasi wote nchini wanaotekeliza mradi wa usambazaji wa umeme vijiji wanatakiwa kukamilisha kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba, hata hivyo serikali imekaririwa ikisemakuwa haitaongeza muda kwa yeyote ambaye atashindwa kukamilisha kazi hiyo na tachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

NAIBU WAZIRI MGALU AKERWA KUSUASUA MRADI WA UMEME JUA KIBITI



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (kulia) akisikiliza maelezo ya Msimamizi wa miradi ya REA, Kanda ya Pwani, Mhandisi Balisidya Myula, kuhusu mradi wa umeme jua unaotekelawa katika kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, Mei 16, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.

Na Veronica Simba – Pwani

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo amekerwa na taarifa za kusucasua mradi wa umeme jua unaotekelawa katika kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, ambapo ameagiza mkandarasi anayesimamia mradi huo, Kampuni ya T & A Business Centre, kuchukuliwa hatua za kisheria.

Akizungumza kijijini hapo baada ya kupokea malalamiko ya kusucasua kwa mradi, kutoka kwa baadhi ya viongozi wa kijiji hicho, Mei 16, 2020, Naibu Waziri, aliutaka Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ambao ndiyo mfadhibili

wa mradi, kuwasilisha wizarani, taarifa rasmi ya utekelezaji wake, ndani ya kipindi kisichozidi wiki moja.

“Taarifa hiyo ibainishe kwanini mradi umekwama, hali iliyo fikiwa na hatua za kisheria zilizochukuliwa,” amesisitiza Naibu Waziri.

Vilevile, Mgalo alikiri kuwa ziara yake mahali hapo ni kufuatia malalamiko hayo yaliyomfikia kuititia kwa viongozi wa eneo hilo akiwemo Mbunge, Diwani na viongozi wa Chama Tawala (CCM).

Maagizo mengine aliyyatao ni kwa REA kuandaa orodha ya miradi yote ya umeme katika maeneo yasiyofikiwa na gridi ya Taifa (Off-Grid) na kuiwasilisha kwenye Mamlaka za Serikali

za Mitaa nchi nzima ili viongozi wajue.

“Viongozi wanapaswa kujua miradi hiyo iko katika hatua gani, imeunganisha wateja wangapi na matarajio/malengo yake ni nini.”

Aidha, aliutaka Wakala huo pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kukaa na Mkandarasi husika na kufanya mapitio ya bei ya umeme huo ili isitofautiane na ile ya umeme wa TANESCO kama ambavyo alielekeza Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani.

Vilevile, Naibu Waziri aliagiza kijiji hicho cha Nyambili, kuondolewa katika orodha ya vijiji vyenye umeme maana kiuhalisia hakina umeme kutokana na idadi ya wananchi waliounganishiwa huduma hiyo kuwa ndogo sana na kwamba hata hao waliounganishiwa hawapati huduma hiyo ipasavyo.

Alishangazwa na kusikitishwa na matumizi

INAENDELEA UK.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (kushoto), akizungumza na baadhi ya viongozi na wawakilishi wa wananchi wa kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa mradi wa umeme jua, Mei 16, 2020.

NAIBU WAZIRI MGALU AKERWA KUSUASUA MRADI WA UMEME JUA KIBITI

INATOKA UK.

11

ya pesa iliyotumika kufadhili mradi husika yasiyowiana na utekelezaji wake ambapo amewataka wataalamu wa Serikali kujenga utamaduni wa kuwajibika kama wanavyotakiwa ili kuhakikisha miradi mbalimbali wanayoismamia inatekelezwa ipasavyo kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Naibu Waziri alionya kuwa Serikali haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu wahusika wote, endapo itatokea tena mahali popote nchini, viongozi wa eneo husika kutokuwa na taarifa ya miradi ya aina hiyo inayotekelawa katika maeneo yao.

Awali, akiwasilisha taarifa ya malalamiko ya kusuasua kwa mradi husika, kwa niaba ya



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo akiangalia moja ya paneli za umeme jua zilizofungwa katika kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, akiwa katika ziara ya kazi, Mei 16, 2020.

wananchi wa eneo hilo, Mtendaji wa Kijiji cha Nyambili, Elia Clement, alibainisha moja ya changamoto

wanazokabiliana nazo ni umeme kupatikana kwa masaa machache kwa siku.

Aidha, alisema tangu kuanza kutekelezwa kwa



Mkazi wa kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, Said Omari akieleza mbele ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani), changamoto za umeme wanazokabiliana nazo kijijini hapo. Naibu Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Mei 16, 2020.



Mkazi wa kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, Haji Ali, akieleza mbele ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo (hayupo pichani), changamoto za umeme wanazokabiliana nazo kijijini hapo. Naibu Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Mei 16, 2020.

mradi huo mwaka 2017, wananchi hawajawahi kupewa taarifa zozote zinazouhusu na wamekuwa wakilazimika kuzitafuta wao wenye kwa njia mbalimbali pasipo kupewa ushirikiano.

Clement alisema hata viongozi wa ngazi mbalimbali ikiwemo kijji, kata na wilaya, hawapewi ushirikiano wa kufahamishwa kuhusu mradi husika.

Akitoa maelezo mbele ya Naibu Waziri, Msimamizi wa miradi ya REA, Kanda ya Pwani, Mhandisi Balisidya Myula alikiri kusuasua kwa Mkandarasi katika kutekeleza mradi husika na kwamba tayari Wakala huo umechukua hatua ikiwa ni pamoja na kumwandikia barua ya kusudio la kutaka kuchukua hatua za kisheria kuhusu mradi husika.

Akieleza zaidi, amesema mkandarasi ameunganisha wateja 10 tu hadi sasa kati ya 34 aliopaswa kuwaunganisha na kwamba kwa mujibu wa mkataba, alipaswa kukamilisha mradi mwanzoni mwa mwaka 2018 lakini hadi sasa hajakamilisha.

Mradi huo umegharimu shilingi 232,170,000 za Tanzania ambazo zilitolewa na wadau wa maendeleo kupitia Wakala huo.

MATUKIO PICHANI

13



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye ushungi-kulia), akizungumza na baadhi ya viongozi na wawakilishi wa wananchi wa Kata ya Nanjirinji, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi, alipokuwa katika ziara ya kazi ambapo alizindua rasmi mradi wa umeme juu, Mei 17, 2020.



Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai akizungumza wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (mwenye kilemba-meza kuu), katika kijiji na Kata ya Nanjirinji, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi ambapo alizindua rasmi mradi wa umeme juu Mei 17, 2020.




Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, Elia Clement (kushoto) akieleza mbele ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (wa kwanza-kulia), changamoto za umeme wanazokabiliana nazo kijijini hapo. Naibu Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Mei 16, 2020.

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umemes Tanzania (TANESCO), wakifuatilia hafla ya uzinduzi rasmi wa mradi wa umeme juu Nanjirinji, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi, uliofanyanya na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Mei 17, 2020.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na baadhi ya viongozi na wawakilishi wa wananchi wa kijiji cha Nyambili, Kata ya Bungu, Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani (hawapo pichani), alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa mradi wa umeme juu kijijini hapo, Mei 16, 2020.



Shehena ya Mafuta ikiwa imepakiwa katika matangi tayari kwa kusafirisha, hapa ni katika ghala la kuhifadhi na kupokea mafuta la kampuni ya GBP mkoani Tanga, Waziri wa Nishari, Dkt. Medard Kalemani, alifanya ziara katika eneo hilo, Mei 10, 2020.

Umeme wa SGR kukamilika mwishoni mwa Mei, 2020

»»» Tanesco kutumia Bil.1.2 kuboresha umeme Kiwanda cha Sukari Mtibwa

**Na Zuena Msuya,
Morogoro.**

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme utakaotumika katika Reli ya kisasa ya kuendesha Treni inayotumia umeme umekamilika kwa zaidi ya asilimia 94 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2020.

Dkt. Kalemani alisema hayo mkoani Morogoro, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme mkubwa, na kusema kuwa ameridhishwa na kasi ya ujenzi huo ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu pamoja na kutembelea Kiwanda cha Sukari Mtibwa kuona hali ya upatikanaji wa umeme, Mei 11, 2020.

Alisema kukamilika kwa

mradi huo kutachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi kwa kuongeza mapato kwa kuwa umeme mwingi utakuwa ukinunuliwa kutoka Shirika la Umeme nchini (TANESCO), vilevile Shirika la Reli nchini (TRL) litapunguza gharama za kununua mafuta ya kuendesha treni.

Njia hiyo ya umeme itapita katika vituo vinne vya njia ya treni ya kisasa ambavyo ni Pugu mkoani Dar es salaam, Ruvu mkoani Pwani, Kidugaro na Kingulwira mkoani Morogoro.

“Mradi huu utakamilika ndani ya muda uliopangwa, kwa sababu tayari nguzo kubwa za umeme 450 kati ya 455 zinazotumika katika ujenzi wa njia hiyo, zimekwisha jengwa na kusalia nguzo tano(5) tu ambazo zinaendelea kujengwa ili kukamilisha ujenzi, hivyo kabla ya mwisho wa mwezi huu, mkandarasi atakuwa amemaliza kazi yote, na

kitakachofuata ni kusubiri kukamilika kwa reli yenye ili tuanze kufanya majoribio ya umeme huo”, alisema Dkt. Kalemani.

Alisema kuwa mradi huo ni wa kwanza kwa nchi za Afrika Mashariki, ukifatiwa na Kenya ambayo imepanga kuanza kuujenga mwakani 2021, na Uganda ambayo imepanga kuanza kuujenga mwaka 2025.

Mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi za kitanzania Bilioni 72.6, na mkandarasi amekuwa akilipwa fedha zake kwa wakati.

Akiba katika Kiwanda cha Sukari Mtibwa, Dkt. Kalemani alisema kuwa serikali imetenga shilingi za kitanzania Bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme utakaokuwa ukitumiwa na kiwanda cha sukari peke yake, katika kuendesha shughuli za uzalishaji.

Njia hiyo ya umeme inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita kuanzia mwezi Mei mwaka huu, ambayo itasaidia kiwanda hicho kupata umeme

mwingi na kutosha kukidhi mahitaji ya kiwanda na ziada kwa zaidi ya miaka mitano ijayo.

“Kilichonileta hapa ni kuwajengea njia ya umeme wenu peke yenu, tumeshakaa na wataalam ili kumaliza tatizo hili, umeme hapa unatoka Msamvu takribani Kilomita 100 na unatumia na watu wengi, fedha tayari imekwisha tengwa na ujenzi utanaza keshokutwa (Mei 13, 2020) ili kukidhi mahitaji yenu ya kutaka umeme takribani Megawati 27 kwa miaka 5 ijayo, sasa lazima tuwape zaidi bila shaka mtatanua kiwanda hichi hapo baadaye,” alisema Dkt. Kalemani.

Kwa sasa kiwanda cha sukari Mtibwa kinapata Megawati 5 hadi 8 ambao pia wakati mwingine unakuwa na nguvu ndogo kutokana na kusafiri umbali mrefu pia umekuwa ukikatika kusababisha uharibifu wa vifaa na kutokidhi mahitaji ya uzalishaji.

Kiwanda hicho lilijengwa mwaka 1954 na kuanza uzalishaji mwaka 1963 hadi sasa, kinauezo wa kuzalisha tani 200 hadi 35 za sukari kwa siku, matarajio ni kuzalisha tani 1000 kwa siku kwa kuwa wanafanya ukarabati na kuboresha miundombinu kiwanda hicho ikiwemo umeme.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akipata maelezo kutoka Msimamizi Mkuu wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa utakaotumika katika reli ya kisasa(SGR) kuendesha treni ya umeme wakati alipofanya ziara ya kukagua njia hiyo, Mei 11, 2020 mkoani Morogoro.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(katikati) akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Umeme wa Kiwanda cha Sukari Mtibwa, mhandisi Juma Palamba (kulia) wakati Waziri alipofanya ziara ya kutembelea kiwanda hicho kufahamu hali ya upatikanaji wa umeme, Mei 11, 2020 mkoani Morogoro.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akikagua baadhi ya maeneo katika cha sukari Mtibwa, alipofanya ziara kiwandani hapo kufahamu hali ya upatikanaji wa umeme, Mei 11, 2020 mkoani Morogoro.

Dkt.Kalemani: Juni 30, 2020, mkandarasi atakayeshindwa kukamilisha REA kukatwa 10% ya malipo yake

Na Zuena Msuya Tanga,

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amesema mkandarasi yeyote aliyepewa jukumu la kutekeleza mradi ya REA akishindwa kukamilisha kazi hiyo ifikapo Juni 31, 2020 kama ilivyoelekezwa katika makubaliano ya mkataba atakatwa asilimia kumi(10%) ya yalipo yake yaliyosalia.

Dkt. Kalemani alitoa kauli hiyo wakati alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa usambazji wa umeme vijijini katika Wilaya za Handeni, Korogwe na Lushoto Mkoani Tanga, Mei 09, 2020.

Alisema kuwa kwa mujibu wa mkataba, wakandarasi wote nchini waliopewa kazi ya kutekeleza mradi wa usambazaji umeme vijijini wanatakiwa kukamilisha kazi hiyo ifikapo mwezi Juni 30,2020, kwa wilaya za mikoa yote nchini, na atakayeshindwa kufanya hivyo mradi huo utakabidhiwa kwa mkandarasi mwagine na atakatwa asilimia kumi (10%) ya malipo yaliyosalia.

Dkt. Kalemani alisisitiza kuwa endapo, mkandarasi atatakwa asilimia kumi (10%) ya malipo yake yaliyosalia,fedha hizo zitapelekwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha,(HAZINA) ili zitumike kumlipa mkandarasi mwagine atakayepewa jukumu la kukamilisha mradi huo.

"Hakuna sababu ya msingi ya kumfanya mkandarasi ashindwe kukamilisha mradi huo kwa mujibu mwa mkataba, pia itanishangaza akishindwa kufanya hivyo kwa sababu fedha zote



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akizungumza na mimoja wa mwenye nyumba katika kijiji cha Kwasunga wilayani Korogwe Mkoani Tanga, baada ya kuwasha umeme katika nyumba hiyo,alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika wilaya hiyo Mei 9, 2020.

za awali walishalipwa na vifaa vyote viro na vinapatikana hapa nchini, tunataka kukamilisha kazi hii ndani ya wakati ili tusonge mbele, kwa hili sitamvumilia yeyote", alisema Dkt. Kalemani.

Katika ziara hiyo Dkt. Kalemani aliwasha umeme katika Kijiji cha Kisasu Kata ya Sindenii wilayani Handeni, pia katika kijiji cha Kwasunga wilayani Korogwe, na katika kijiji cha Kwamsale Kata ya Emtoye wilayani Lushoto mkoani Tanga.

Aidha aliaagiza Viongozi wa Serikali za Mitaa waliofika katika shughuli za uwashaji umeme kwa niaba ya wananchi wao,ili kuепuka mikusanyiko isiyo ya lazima ikiwa ni tadhadari ya kujikinga na maambuki ya Corona, kuwashimiza na kuwasisitiza wananchi wao kuendelea kulipia gharama za kuunganishwa umeme ya shilingi 27,000 tu .

Pia wasikubali kulipia miundombinu ya umeme kama, nguzo, nyaya, mita za luku na mashineumba kwakuwa tayari zimekwisha lipiwa na serikali.

Katika ziara hiyo pia

alitembelea Kituo cha Kupoza na Kusambaza umeme cha Kilole kilichopo wilayani Korogwe mkoani Tanga, kilichojengwa mwaka 1929 chenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2.5 ambacho kwa sasa kinafanyiwa ukarabati mkubwa.

Dkt. Kalemani aliuagiza uongozi wa Shirika la Umeme Nchini(TANESCO) kukamilisha ukarabati huo ifikapo June 15, 2020, mwaka huu ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa umeme kwa wakazi wa Walaya ya Korogwe mkoani humo.

Vilevile aliuagiza TANESCO kutafuta eneo kubwa zaidi ili kukihamisha kituo hicho ambacho kiko katika eneo finyu na kimezingirwa na makazi ya watu.

Alisema kuwa endapo kituo hicho kitahamishiwa katika eneo kubwa zaidi kitakuwa na fursa ya kuongezewa uwezo zaidi na hata kujengwa mitambo mingine mikubwa ya kupoza na kusambaza umeme kwa watumizi mengine hapo baadaye.

Ukarabati unaofanyika katika kituo hicho ni kufunga mashineumba

mpya yenye uwezo wa kuzalisha Megawati tano za umeme, kuweka vifaa na miundombinu mipy ya kituo hicho pamoja na kutenganisha njia za kusafirisha umeme kutoka katika kituo hicho kwenda kwa watumiaji.

"Mnasubiri nini kufunga hii mashineumba ambayo imefika hapa miezi miwili iliopita? ,pia harakisheni ukarabati kwa kubadilisha miundombinu ya kituo hichi, iliopo hapa ni chakavu si mnaiona na niyazamani sana jamani,wananchi watanga wanataka umeme mwangi na wa uhakika, na marufuku kumatika umeme kwa mkoaa huu mara baada ya kukamilika kazi hii", alisisitiza Dkt. Kalemani.

Kuhusu suala la wizi wa umeme na miundombinu yake, Dkt. Kalemani alisema kuwa yeyote atayebainika kufanya vitendo vya wizi ni muhujumu uchumi hivyo achukuliwe hatua za kisheria.

Aliwataka wananchi kwa kushirikiana na mamlaka husika kulinda miundombinu ya umeme

Dkt.Kalemani: Juni 30, 2020, mkandarasi atakayeshindwa kukamilisha REA kukatwa 10% ya malipo yake

INATOKA UK.

16

pia kuwaweka bayana na kuwataja wale wote wenye tabia ya wizi ili wachukuliwe hatua, kuepuka kuleta usumbufu kwa wananchi kwa kukosa huduma ya umeme

na hasara kwa serikali. Sambamba na hilo aliwataka watumishi wa TANESCO kuwa na weledi na wazalendo wakati wa kutekeleza majukumu yao kwa kuwa baadhi yao huchafua sifa za shirika hilo kwa kijihusisha na vitendo vya wizi kwa kushirikiana na watu

walionje ya shirika hilo. Kwa upande wao wakuu wa wilaya za mkoa huo, akiwepo Mkuu wa wilaya ya Handeni Godwin Gondwe, Katibu Tawala, Rahel Muhando kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Korogwe na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Januari

Lugangika, walimuahidi Dkt. Kalemani kuyafanya kazi na kutekeleza maagizo aliyyoatoa, kwa lengo la kuhakisha wananchi wote wanapata umeme utakaochocha shughuli za kiuchumi na maendeleo kwa jumla.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(katikati) akiwasili katika Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga kwa ziara ya kikazi ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini, Mei 9,2020, wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(kulia),Katibu Tawala wa Wilaya ya Korogwe, Rahel Muhandu(kushoto) kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, wakikagua kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kilole wilayani Korogwe, Mei 9,2020, kituo hicho kilijengwa 1929 kwa sasa kinafanyiwa ukarabati kuboresha utendaji kazi wake.



Muonekano wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kilole wilayani Korogwe mkoani Tanga kilichojengwa mwaka 1929, chenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2.5 za umeme ambacho kwa sasa kinachofanyiwa ukarabati.



Baadhi ya Watendaji wa Wilaya ya Handeni, Wakandarasi wanaotekeliza mradi wa usambaji wa umeme vijijini wilayani humo pamoja na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zilizochini yake,wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kabla ya kuanza ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini katika wilaya hiyo, Mei 9,2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani(kushoto) akitoa maeleko kwa msimamizi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kilole,wilayani Korogwe mkoani Tanga, Mhandisi Peter Magari, wakati waziri wa Nishati alipofanya ziara ya kushtukiza kutembelea kituo hicho kilichojengwa 1929 ambacho kinafanyiwa ukarabati kubosha utendaji kazi wake.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akiwasha umeme katika moja ya nyumba za Kijiji cha Kwasunga wilayani Korogwe mkoani Tanga alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya utekelzaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini, Mei 09, 2020.

Dkt. Kalemani aweka historia Loya, Tabora, wakazi wamshukuru kwa kuwashaa umeme

Na Zuena Msuya Tabora,

Wakazi wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui mkoani Tabora, wameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuwaunganisha na kuwawashia umeme katika kijiji hicho ambacho awali wakazi hao walikuwa wakiona kama ni ndoto.

Wakazi hao, wameeleza hayo baaada ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kuwashaa umeme katika kijiji hicho na kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini katika wilaya hiyo, Mei 19, 2020.

Wakazi wa Kijiji hicho walisema kuwa, miaka mingi wamekuwa wakipewa ahadi zisizotekelzeza na wakati mwingine wamekuwa wakikatishwa tamaa ya kupata umeme kwa kuwa kijiji hicho kiko umbali mrefu kutoka ilipo miundombinu ya umeme pia kuwa na jiografia isiyorafiki kufika maeneo hayo.

"Huyu Waziri ameandika historia hapa Loya, haijawahi kutokea kiongozi mkubwa ngazi ya Waziri kufika katika kijiji chetu tangu kimeanzishwa, wengi wanakuja katika wilaya hii lakini wanaishia huko mujini tu vijijini hawafiki, na amekuja kutuwashia umeme kabisa kwakweli tunamshukuru sana huyu Dkt. Kalemani, pia tunamshukuru Rais Magufuli kumkubalia huyu waziri kuja huku kwetu kutuletea umeme, abarikiwe sana", alisema mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Josephat Wamalulu.

Kwa upande wake Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, (kulia) akiteta jambo na Mbunge wa Igalula, Musa Ntimizi (kushoto), wakati alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini na kuwashaa umeme katika baadhi ya nyumba za wakazi wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora, Mei 19, 2020.

alisema baada ya kusikia malalamiko na kuona uhitaji mkubwa wa umeme kwa kijiji hicho ambapo bado hakiifikiwa na mradi wa kusambaza umeme (REA) kwa kipindi hiki, nililiagiza Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) kupeleka umeme kwa gharama zao katika kijiji hicho.

Alisema kijiji cha Loya kinawakulima wengi wa mpunga, karanga na wafanyakishara ambao wanahitaji huduma ya umeme katika kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Kwa mantiki hiyo, TANESCO ilitenga zaidi ya shilingi Bilioni 3 ili kuhakikisha umeme unafika katika kijiji hicho, ambacho kiko umbali mrefu sana kutoka ilipopita miundombinu ya umeme.

"Nililiagiza TANESCO kuleta umeme hapa Loya, kama mlivyoona Loya inawakazi wengi wakulima na wafanyakishara ambao wanahitaji umeme katika shughuli zao, tumetenga zaidi ya shilingi Bilioni

tatu kuhakikisha umeme unafika hapa na tutapeleka katika vijiji vingine cha msingi hapa ni ninyi wananchi kusuka nyaya katika nyumba zenu, na kulipia shilingi 27,000 tu umeme utawafikia", alisema Dkt. Kalemani.

Aidha aliwaagiza TANESCO, kuendelea kusambaza na kuwashashaa umeme kwa wakazi wa eneo hilo waliokwisha kulipia gharama za kuunganishiwa umeme ndani ya siku 7 baada ya kulipia.

Aliwataka wakazi wa Loya kutumia umeme huo kujiendeleza kiuchumi badala ya kuutumia umeme huo kwa kuwashaa taa peke yake.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Igalula, Musa Ntimizi aliwataka wafanyakishara katika kijiji hicho kutanua wigo wa kibashara na wakulima wa mpunga kuongeza thamani ya mazao yao ili kupata faida zaidi.

Pia wakazi hao

wachangamkia fursa hiyo ya umeme kwa kuazisha biashara na viwanda vidogo vinavyotumia umeme, kama vile Saloni, Mashine za kusaga na kukoboa nafaka, kuchomelea vyuma na kadhalika.

"Umeme huu umekuja wakati muafaka kwa wakazi wa Loya, sasa hivi tutaanza kuuza mchele safi na bora badala ya mpunga ambao hata hivyo wafanyakishara kutoka nje ya hapa walikuwa wakiwalangua kwa wakulima wa eneo hili, sasa hivi kutakuwa na mashine za kisasa za kukoboa mpunga na wakulima wataongeza thamani ya mazao yao na kunufaika zaidi na kilimo cha mpunga", alisema Ntimizi.

Aliwaeleza wakazi hao kuwa wasikubali kuuziwa nguzo za umeme, pia watumie wakandarasi waloidhinishwa na TANESCO kufanya kazi ya kutandaza nyaya katika nyumba zao ili kuuepuka vishoka.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, akiwaonyesha kifaa cha Umeme tayari (UMETA) wakazi wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, katika kijiji hicho, Mei 19, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, akiwashasha mashine ya kusaga na kukobia nafaka ambayo sasa inatumia umeme badala ya mafuta mazito kuijidesha, inayomilikiwa na Mkazi wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora, wakati alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, katika kijiji hicho, Mei 19, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, (katikati), Mbunge wa Igalula, Musa Ntimizi na Viongozi wengine walioambatana nao wakipita katika mitaa ya Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora, walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, katika kijiji hicho,na kuwashasha umeme Mei 19,2020.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani, akiwashasha umeme katika moja ya Ofisi za Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora, wakati alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, katika kijiji hicho, Mei 19, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt.Medard Kalemani,(kushoto) akiwashukuru wakazi wa Kijiji cha Loya wilayani Uyui Mkoani Tabora,baada ya kumkabidhi zawadi ya Ng'ombe(kulia) ili aifikiše kwa Rais wa Nchi, Dkt. John Magufuli kwa kuwapatia umeme katika kijiji hicho, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini, katika kijiji hicho, Mei 19,2020.

EWURA yapewa siku 10 kupitia bei za mafuta katika maghala ya kuhifadhi na kupokea mafuta

Na Zuena Msuya Tanga,

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, ametoa siku kumi kwa Mamlaka ya Udhibiti huduma za Nishati na Maji (EWURA) kumpatia majibu ya uwiano wa viwango vya bei ya mafuta katika maghala ya Kupokea na kuhifadhia mafuta nchini.

Dkt. Kalemani alisema hayo alipofanya ziara ya kutembelea ghal la kuhifadhia mafuta la kampuni ya GBP iliyoko mkoani Tanga, Mei 10, 2020, ili kuona kama agizo lake alilolitoa mwezi Machi, 2020, la kuwataka waagizaji mafuta nchini wanaagiza shehena kubwa kutokana na tishio la kuwepo kwa virusi vya Corona.

Pia alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini katika wilaya ya Mkinga na Muheza mkoani huo pamoja na kuwashaa umeme.



Waziri wa Nishari, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela (kulia) wakiteta jambo baada ya waziri wa nishati, kufanya ziara katika ghal la kuhifadhi na kupokea mafuta Kampuni ya GBP mkoani Tanga, Mei 10, 2020.

Baada ya kupata taarifa ya mwenendo wa uingizaji, upokeaji na uhifadhi wa mafuta nchini katika maghala

pamoja na mambo mengine, Dkt. Kalemani aliiagiza EWURA kufanya tathmini ya bei ya mafuta katika maghala hayo

kwa lengo la kuboresha biashara ya mafuta kwa maslahi ya watumiaji na

INAENDELEA UK.

21



Kamishna wa Maendeleo Petroli wa Wizara ya Nishati, Adam Zuber (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa pamoja nchini (PBPA) erasto samwel (katikati) walimsikiliza Waziri wa Nishari, Dkt. Medard Kalemani, (hayupo pichani) akizungumza baada ya kufanya ziara katika ghal ya kuhifadhi na Kupokea mafuta Kampuni ya GBP mkoani Tanga, Mei 10, 2020.



Waziri wa Nishari, Dkt. Medard Kalemani (wa pili kulia) akipita kukagua mazingira ya ghal la kuhifadhi na kupokea mafuta la kampuni ya GBP, alipofanya ziara katika eneo hilo mkoani Tanga, Mei 10, 2020.

EWURA yapewa siku 10 kuitia bei za mafuta katika maghala ya kuhifadhi na kupokea mafuta

INATOKA UK.

20

wafanyabiashara.

Dkt.Kalimani alisema kuwa, serikali imeweka utaratibu wa kuweka maghala ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika kila ukanda wa nchi kwa lengo la kuwapunguzia gharama za usafiri wafanyabiashara wa mafuta wanaotembea umbali mrefu kuyafuata mafuta hayo, pia kuwezesha watumiaji kupata huduma hiyo kwa haraka, karibu na kwa bei nafuu wakati wote.

Sambamba na hilo kulinda ubora wa miundombinu ya barabara nchini kwa kuwa magari yanayobeba mizigo mizito ikiwemo mafuta yamekuwa yakichangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa barabara.

"EWURA na PBPA nawapa siku 10,muangalieni uwiano na uratibu sahihi wa bei ya mafuta katika maghala ili bei hizo zisitofautiane sana na taratibu za bei zilizowekwa, kwa kuwa mafuta yapo mengi nayakutoshwa, na mnilettee majibu, Lengo la serikali ni kuhakikisha mafuta yanapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu wakati wote kwa kuwanufaisha wafanyabiashara na watumiaji", alisema Dkt. Kalemani.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wa mafuta kwa kanda ya kaskazini ikiwemo Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga kutumia ghalaa la kuhifadhi na kupokea mafuta lililopo mkoani Tanga kuliko kuyafuata mkoani Dar Es Salaam. "Wafanyabiashara

wanaofuata mafuta Dar es salam watalazimika kuuza kuwauzia watumiaji kwa bei ya juu hivyo kuwakandamiza watumiaji hii si sahihi na ndio maana karibu kila ukanda wa nchi tumeweza ghalaa la kuhifadhi na kupokea mafuta,tofauti na ilivyokuwa awali mafuta yote yalikuwa yakipatikana mkoani Dar Es Salaam pekee",alisitiza Dkt. Kalemani

Alitoa wito kwa makampuni yote ya uwagizaji wa mafuta nchini kwa kushirikiana na EWURA na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (PBPA)kushirikiana kwa pamoja kuendelea kuleta mafuta mara dufu ili kujihakikishia uwepo wa mafuta nchini hata kama ugonjwa wa corona utaendelea kuwepo.

Dkt. Kalemani alifanua kuwa mafuta yaliyopo nchini kwa sasa yanauwezo wa kutumika zaidi ya miezi miwili hadi mitatu mbele na bado kila siku wanapokea mafuta, ambapo kwa sasa nchi inapokea inapokea mafuta lita milioni 428.7 tofauti na awali kabla ya agizo kutoka ilikuwa ikipokea mafuta lita milioni 185.

Aidha aliwataka wafanyabiashara ya mafuta kujenga vituo yva mafuta katika maeneo yaliyo vijijini ili kulinda ubora wa mafuta na kusogeza huduma karibu na watumiaji hasa wadogo akitolea mfano waendesha pikipiki ambaa ndio wanaotegemeo kubwa la usafiri katika maeneo ya vijijini.

Alisema kuwa watumiaji wadogo wa vyombo vya moto, wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kutafuta

huduma ya mafuta, na wengine wamekuwa wakihifadhi mafuta katika nyumba zao jambo ambalo linahatarisha usalama wao.

Aidha alisema kuwa pia kumekuwa na tabia ya kuuza kiholela mafuta na uhifadhi mbovu wa mafuta hayo na hivyo kupunuza ubora wawiwango vya mafuata kwa watumiaji na hivyo hata kulazimu mafuta hayo kuchanganya na hivyo kuchangi uharibifu wa vyombo vinavyotumia mafuta hayo.

"Wafanyabiashara nendeni mkajenge vituo vidogo vya mafuta vijijini, mrahisishe huduma ya upatikanaji wa mafuta na bei nafuu kwa watumiaji wadogo ambaa wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo,tuungane kutekeleza lengo la serikali la kuhakikisha kila mtumiaji wa mafuta anapata bishaa hiyo kwa wakati na kwa bei nafuu", alisitiza Dkt. Kalemani.

Pamoja na mambo mengine alitembelea eneo inapojengwa kifaa kitakachotumika kupima mafuta (Flow Meter), yanayoingia nchini kutoka katika Meli kwenda katika maghala ya kuhifadhi na kupokea mafuta katika Bandari ya Tanga.

Aliagiza mamlaka ya bandari nchini kukamilisha ujenzi wa mtambo huo haraka ili serikali ipate kiwango sahihi cha mafuta yanayoingia nchini kuitia Bandari ya Tanga ili kupata kodi na tozo stahiki.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Uagizaji mafuta ya GBP, Badar Seif Sood alimueleza Waziri wa Nishati kuwa wamefanya upanuzi wa bandari hiyo,

hivyo kwa sasa inauwezo wa kuhifadhi na kupokea mafuta lita milioni 182, tofauti na walivyokuwa wananza mwaka 2017 walipokuwa wakihifadhi na kupokea mafuta lita milioni 182, na upanuzi utaendelea kulingana na mahitaji.

Aliishukuru serikali kuitia wizara ya nishati, kuendelea kuwalinda wafanyabiashara wa mafuta wakiwamo wamiliki wa maghala ya kuhifadhi na kupokea mafuta pamoja na waagizaji wakubwa wa mafuta kwa kuhakikisha wanafanya biashara zao katika mazingira rafiki: Huku akiahidi kuendelea kutoa huduma bora kwa watumiaji wa mafuta hayo nchini.

Katika ziara hiyo, Dkt. Kalemani, pia alikagua maendeleo ya usambazaji wa umeme vijijini katika Wilaya ya Mkinga na kuwashaa umeme katika kijiji cha Mbuyuni kata ya Mapatano na kutembelea kisima cha maji katika kijiji cha Jihirini na kuliagiza Shirika la Umeme nchini (TANESCO), kupeleka na kuwashaa umeme katika kisima hicho mwishoni mwa mwezi huu.

Vilevile alitembelea Wilaya ya Muheza na kukagua kazi ya usambazaji wa umeme katika kijiji cha Kwakokwe na kuwataka wananchi kuendelea kulpia gharama za kuunganishiwa umeme kwa kuwa vijijini vyote nchini vitapata umeme na kwamba wasikubali kuuza wa miundombinu ya umeme na pia watumie wakadarasi wanaotambulika na TANESCO katika kutandaza nyaya katika nyumba zao.

MATUKIO PICHANI

22

Shehena ya
Mafuta ikiwa
imepakiwa
katika matangi
tayari kwa
kusafirishwa, hapa
ni katika ghala
la kuhifadhi na
kuopeka mafuta la
kampuni ya GBP
mkoani Tanga,
Waziri wa Nishari,
Dkt. Medard
Kalemani, alifanya
ziara katika eneo
hilo, Mei 10, 2020.



Baadhi ya mapipa makubwa ya
kuhifadhi mafuta katika ghala
la kuhifadhi na kuopeka mafuta
la kampuni ya GBP mkoani
Tanga, Waziri wa Nishari, Dkt.
Medard Kalemani, alifanya ziara
katika eneo hilo, Mei 10, 2020.



Muonekano wa eneo kitakapojengwa kifaa cha kupimia mafuta
(Flow Meter) kutoka katika meli hadi katika maghala ya kuhifadhi
na kuopeka mafuta katika bandari ya Tanga, Waziri wa Nishati,
Dkt. Medard Kalemani, alifanya ziara katika eneo hilo, Mei 10, 2020.

Waziri wa Nishari, Dkt. Medard Kalemani, (katikati) akiwasha
umeme katika moja ya Ofisi za Serikali ya Kijiji katika Kijiji cha
Mbuyuni Kata ya Mapatano wilayani Mkinga, mkoani Tanga,
alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme
vijijini katika wilaya hiyo, Mei 10, 2020.

TANESCO KATENI UMEME KWA WADAIWA SUGU MUONGEZE MAPATO – DKT. KALEMANI



Zuena Msuya - Dodoma

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuendelea kukata umeme kwa wadaiwa sugu ili kukusanya mapato zaidi na kulipa madeni ya shirika hilo.

Dkt. Kalemani alisema hayo Aprili 30, 2020, jijini Dodoma, alipokutana na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa TANESCO, kuzungumzia tathmini ya miaka mitano ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu.

Katika kikao hicho, mambo mbalimbali yalijadiliwa kuhusiana na nishati ya umeme inayozalishwa nchini kwa lengo la kuleta manufaa makubwa zaidi kiuchumi

nchini, TANESCO na watumiaji wa umeme huo ikiwemo viwanda, wafanyabiashara na matumizi mengine.

Dkt. Kalemani aliagiza TANESCO kulipa madeni yote inayodaiwa na kutoongeza madeni mapya, vilevile wadaiwa sugu wakumbushwe madeni yao na endapo hatalipwa, shirika hilo liwakatie umeme kwani kufanya hivyo kutamaliza tatizo la wadaiwa sugu.

Alisema TANESCO inadaiwa madeni makubwa, pia ina wateja wengi sana ambaa ni wadaiwa sugu wanaodaiwa fedha nydingi sana na hawalipi, zikiwemo taasisi, mashirika ya umma na binafsi, pamoja na watumiaji wa kawaida.

"Ninawaagiza TANESCO nendeni mkawakatie umeme! Narudia tena mkakate umeme! Mkishaukata, wahusika watalipa na wataonyesha ushirikiano mkubwa, tofauti

na kumdati kawaida tu," alisema Dkt. Kalemani.

Kuhusu wizi na uhujumu wa miundombini ya umeme, Dkt. Kalemani, alitaka TANESCO, Bodi ya TANESCO na Watendaji wa Wizara ya Nishati, kushirikiana kwa pamoja kutafuta njia sahihi na ya kisasa zaidi ya kubaini wizi wa umeme unaofanywa na watu wasio waaminifu na kusababisha hasara kwa shirika na kupoteza mapato ya taifa.

"Wizi wa umeme upo na haukubaliki, tuweke mfumo sahihi wa kisasa kubaini wahusika. Vilevile tuwe na walanzi wenye weledi katika miradi yetu bila kujali ni ya serikali au mtu binafsi. Jukumu la ulinzi ni letu sote kwa faida ya Taifa kwa jumla," alisitisiza Dkt. Kalemani.

Aidha, aliwataka kuendelea kufanya tathmini na uwiano wa gharama za kutengeneza nguzo za zege na nguzo zinazotumika sasa,

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mbele-kushoto) akiwa ameambatana na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO, kukagua shughuli za ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, Aprili, 30, 2020. Katikati ni Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalo.

ili kuangalia uwezekano wa kutumia nguzo za zege katika maeneo yote nchini lakini kwa gharama nafuu, kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya kuoza ama kuungua kwa nguzo katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo aliweka wazi kuwa katika baadhi ya maeneo ambayo ni korofii nguzo za zege zimeanza kutumika japo ni za gharama kubwa.

Vilevile, alitaka kuongezeka kwa idadi ya wateja wa umeme katika kila sekta, kuharakisha uunganishaji wa umeme kwa mteja pale anapomaliza kulipia gharama husika, pamoja na kutatua changamoto za wateja kwa wakati sahihi ili kuvutia wateja wengi zaidi na kuondoa malalamiko.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo aliwataka TANESCO kuangalia uwezekano wa kutoa zawadi kubwa kwa wasamaria wema wanaotoa taarifa za siri kuhusu wanaohujumu na kuiba umeme tofauti na ile inayotolewa sasa, ambayo pia huchukua muda mrefu kuiqidhi kwa muhusika.

Mgalu alikitaka kitengi husika kutunza siri za watoa taarifa, pia kufanya uchunguzi wa kina na kutoa adhabu kwa mtumishi yeoyote atakayetiliwa

TANESCO KATENI UMEME KWA WADAIWA SUGU MUONGEZE MAPATO – DKT. KALEMANI

INATOKA UK.

23

shaka, au kuhusika na wizi pamoja na kuhujumu miundombinu ya umeme kama inavyofanywa kwa wahusika wengine wanaobainika.

Vilevile, alitaka kuwe na uhamasishaji wa kuwavutia watoa taarifa ili kupata matokeo chanya kuhusu wizi na uhujumu wa miundombinu ya umeme, watashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuimarisha ulinzi kuanzia ngazi za kaya.

Mhandisi Said, alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kubaini wezi na wahujumu wa miundombinu ya umeme kwa kuwa watu hao wasio wazalendo huwa



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye kofia nyeupe) akiwa na Wajumbe wa Bodii ya Wakurugenzi ya TANESCO. Hapa akimweleza jambo Mwenyekiti wa Bodii hiyo, Dkt. Alexander Kyaruzi (kushoto) walipotembelea eneo la kuhifadhi nguzo za umeme wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kufua umeme cha Zuzu jijini Dodoma, Aprili 30, 2020.

wanaonekana na hata kufahamika katika maeneo yao.

Mwenyekiti wa Bodii ya Wakurugenzi wa TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi, alishuruku Wizara ya Nishati kwa kuwapa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yao na kuyafanya kazi yale waliyokuwa wakiishauri wizara hiyo, katika kipindi chote cha miaka mitano.

Dkt. Kiyarunzi, alikiri kuwa kazi ya kusambaza umeme siyo jambo jepesi, hivyo wanajivunia kuona maendeleo makubwa katika sekta ya nishati ya kuongeza wigo wa usambazaji wa umeme vijijini, kujenga miradi mikubwa ya kuzalisha, njia za kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vyya kupoza na kusambaza umeme nchini.

Awali, kabla ya kufanya kwa kikao hicho,



Vijana wakiendelea na kazi ya ujenzi katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani na Wajumbe wa Bodii ya wakurugenzi ya TANESCO kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo hicho Aprili 30, 2020.

Uongozi wa Wizara na Wajumbe wa Bodii hiyo walifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa upanuzi wa Kituo kikubwa zaidi nchini cha Kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu kilichopo jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Dkt. Kalemani, ujenzi wa kituo hicho utakamilika hivi karibuni na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 648 za umeme.

Aidha, alisema kituo hicho kitaimarisha upatikanaji wa umeme kwa jiji la Dodoma ambalo linaendelea kukua kwa kasi na kitakuwa ndiyo kitovu cha vituo vyote vyya kupoza na kusambaza umeme katika mikoa yote nchini na kupeleka nchi jirani pale itakapohitajika kufanya hivyo.

MATUKIO PICHANI

25

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO wakipata maelezo kutoka kwa Msimamizi Mkuu wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, katika ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo hicho, Aprili 30, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO (hawapo pichani) baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, Aprili 30, 2020. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo na kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said.

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO baada ya ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, Aprili 30, 2020. Kulia ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalo na kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja.



Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) baada ya ziara ya kukagua ujenzi wa upanuzi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Zuzu jijini Dodoma, Aprili 30, 2020.

TANZANIA YATINGA ULINGO WA KIDUNIA WA MABWAWA YA KUZALISHA UMEME WA MAJI

Zuena Msuya - Dodoma

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani amesema kuwa Tanzania imeingia katika ulingo wa Kidunia kutokana na ujenzi wa Bwawa kubwa la kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji katika Bonde la Mto Rufiji wa Julius Nyerere (JNHP) kwa kushika nafasi ya 70 kati ya mabwawa yote ya aina hiyo duniani.

Dkt. Kalemani alisema hayo wakati wa mahojiano yake na Mtangazaji wa Televisheni ya Taifa (TBC1) wakati wa kipindi cha Tanzania Mpya kilichorushwa hewani, Aprili 21, 2020.

Katika mahojiano hayo, Dkt. Kalemani alisema kuwa ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere, umeitambulisha na umeiwezesha Tanzania kuingia katika historia ya Dunia kwa kudhamiria na kutekeleza ujenzi wa mradi huo mkubwa ambao ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 za umeme.

Aliweka wazi kuwa JNHP, linashika nafasi ya nne Afrika, la kwanza likiwa ni la Renaissance lililopo Ethiopia linalozalisha megawati 6450, la pili ni Mambila nchini Nigeria (megawati 3050), la tatu ni Kakula Kabako nchini Angola (megawati 2170) na katika Ukanda wa Afrika Mashariki linashika nafasi ya kwanza.

"Tanzania kwa sasa tumeingia katika nafasi kubwa sana Duniani na Afrika. Kukamilika kwa mradi huu kutatufanya Watanzania tujamini kwa kuwa na uchumi wa viwanda. Aidha, Mradi huu utakamilika kwa wakati, kwa sababu mpaka sasa, Mkandarasi ameshavuka

asilimia 78 ya utekelezaji wa mpango kazi wake," alisema Dkt. Kalemani.

Alisema kuwa baadhi ya watu walikuwa na wasiwasi kuwa Serikali itashindwa kumlipa Mkandarasi! "Sasa nawapa taarifa kuwa mkandarasi ameshalipwa ndani ya wakati kiasi cha shilingi trilioni 1.19 kama malipo ya awali ikiwa ni asilimia 18.8 ya malipo yake yote. Kulingana na Mpango Kazi wake ni asilimia 100 ya malipo aliyotakiwa kulipwa kwa sasa. Ni jambo la kujivunia sana kuwa serikali hajashindwa na haitashindwa kumlipa. Italipa na mradi utakamilika kwa wakati kwa pesa za watanzania," alisitisiza Dkt. Kalemani.

Alitaja baadhi ya mabwawa yaliyopo katika baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kuwa ni pamoa na Kaborabasa la Msumbiji linalozalisha megawati 1,245, Kafue Gorge nchini Zambia litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 1,145 pindi litakapokamilika mwaka 2024, na Karuma nchini Uganda linalozalisha megawati 600.

Katika mahojiano hayo, pia alizungumzia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 400) kutoka eneo la uzalishaji umeme katika bwawa hilo hadi kuwafikia watumiaji, yenyе urefu wa Kilometra 167 hadi Chalinze na ujenzi wake umeshaanza kutekelezwa.

Alifafanua zaidi kuwa baada ya umeme huo kufika Chalinze utaungana na ule wa njia kubwa ya kusafirisha umeme nchi nzima kwenda mkoani Dodoma na kusambazwa pande zote za nchi.

Pili ni kutoka Kibiti Wilayani Rufiji Mkoani Pwani kuititia Mloka mkoani Morogoro yenyе urefu wa Kilometra 210 ya kusafirisha

Megawati 400 za Umeme, ambayo itaanza kujengwa hivi karibuni.

Mradi huo utakapokamilika utawezeshanija zote nne kuu za nchi kuunganishwa ili kuweza kuwapelekea watanzania wote na kuuza katika nchi jirani pale itakapohitajika kufanya hivyo.

Vilivile Dkt. Kalemani alizungumzia mtandao wa ujenzi wa njia kubwa za kusafirisha umeme wa Kilovolti 400 nchini, ambapo alisema kuwa tayari njia ya kusafirisha umeme huo yenyе urefu wa Kilometra 670 kutoka mkoani Iringa kuititia Dodoma, Singida, Shinyanga na Kanda ya Ziwa ukiwemo Mkoaa wa Mwanza imeshakamilika tangu mwaka 2016.

Alisema njia nyingine ya Kilovolti 400, ni ya kutoka Iringa, Sumbawanga, Mpanda, Katavi hadi Kigoma yenyе umbali wa Kilometra 1848, utaratibu wa ujenzi umeanza kwa kipande cha kutoka Iringa hadi Sumbawanga, na tayari Serikali imeshatoa fedha kiasi cha dola milioni 455 kuanza kutekeleza mradi huo.

Vilevile njia hiyo itatoka Kigoma hadi Nyakanazi umbali wa Kilometra 280, pia Geita umbali wa Kilometra 130 na kufika Bulyanhulu umbali wa Kilometra 53, kwa lengo la kuunganisha mtandao wa umeme mkubwa kwa pande zote za nchi, mradi huo utakamilika ndani ya miaka miili ijayo na fedha zipo.

"Hii lazima watanzania mfahamu kuwa kwa mara ya kwanza tumeanza kuwa na mtandao mkubwa wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa Kilovolti 400, utakaotumika katika aina zote za viwanda vinavyojengwa, huu umeme ni kwa matumizi yote, Viwanda, shughuli za kiuchumi na kijamii,

majumbani nakadhalika", alisema Dkt. Kalemani.

Kuhusu Gridi ya Taifa, Dkt. Kalemani alisema kuwa kwa sasa inajengwa Gridi ya Taifa ya ukubwa wa Kilovolti 400 kutoka Dodoma, itakayounganisha nchi ya Zambia kuititia Sumbawanga, pia kutoka Dodoma kuititia Singida, Manyara, Namanga hadi Isinya nchini Kenya, umbali wa Kilometra 512, kwa gharama ya Dola za Marekani 258.24 zitatumika kutekeleza mradi huo ambao utekelezaji wake unaendelea vizuri na utakamilika mwishoni mwa mwezi Mei Mwaka huu 2020. Mradi huo unajulika kwa jina maarufu ZTK kwa maana ya Zambia, Tanzania na Kenya.

Nyingine ni kutoka Dar Es Salaam, Chalinze hadi Segera, Tanga hadi Namanga na kutoka Mwanza kuititia Ziwa Victoria hadi Masakaya nchini Uganda.

Pia alisema kuanzia mwakani kutajengwa mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 300, na njia ya kusafirisha umeme kwenda nchini Msumbiji ili nchi hiyo itakapohitaji umeme iwe rahisi kuwauzia.

"Huu ni mkakati wa kuhakikisha kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa JHPP, umeme wote utakaozalishwa nchini unakuwa mwingi, wakutosha na kwa gharama na nafuu, na ziada inauzwa katika nchi jirani pale watakapohitaji kuititia njia hizo kubwa ambazo zimejengwa", alifafanua Dkt. Kalemani.

Lengo la Serikali ni kuwa na umeme mwingi, wakutosha kwa matumizi ya ndani na ziada kuu nje kutokana na mahusiano mazuri na nchi jirani ikiwemo Uganda, Burundi, Rwanda ambao bado umeme wao hauko imara sana.

MAFANIKIO YA AWAMU YA TANO KWENYE SEKTA YA UMEME

Hafsa Omar

Nishati ya umeme nchini, inategewa na watananza wengi hasa katika shughuli za kiuchumi ambapo Serikali imeweza kuunganisha umeme wateja wapya 1,293,528 na kufanya jumla ya wateja walionganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2020 kufikia 2,766,745, ambayo ni juhud kubwa iliyo fanywa na Serikali ya Awamu wa tano ya kuhakikisha kila mtanzania nafikiwa na umeme wa uhakika.

Hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika siku hadi siku. ambapo kwa sasa umeme wa kutosha unapatikana nchini. Mwaka 2015 kulikuwa na megawati 1,038 za umeme katika gridi ya Taifa. Lakini kwa sasa kuna jumla ya megawati 1,602.34. Zaidi ya megawati 480 mpya zimeongezeka na nchi imekuwa na ziada ya umeme usiopungua megawati 325 kila siku. Miundombinu ya uzalishaji umeme imeimarishwa kwa kuongeza njia kuu za kusafirisha umeme ambazo hazikuwepo huko nyuma. Mwaka 2016 mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 ulikamilika kujengwa, mradi wenye umbali wa kilomita 670 kutoka Iringa kuititia Dodoma - Singida Shinyanga.

Pia, Mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 220 kutoka Makambako kuititia Madaba hadi Songea, umbali wa kilomita 250 nao ulikamilika.

Serikali imeendelea na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme wa (kilovoti 132) mahala ambapo hazikuwepo kabisa mathalani kutoka Mbaga - Mkuranga - Nanjilini Mtwara kuititia Lindi, umbali wa kilomita 5.2.

Aidha katika kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana nchini Serikali kuititia Wizara ya Nishati imeweza kuunganisha maeneo mengi ambayo hayakuwa kwenye gridi ya Taifa, hasa yaliyokuwa yanatumia mashine za kufua umeme wa mafuta.

Ambapo takribani vituo 12 viliviyokuwa vikitumia mafuta ambavyo baadhi yake ni Ngara, Biharamulo, Songea, Mbanga, Namtumbo, Ludewa na Nyakato kwa sasa vimeondolewa katika mfumo huo wa utumiaji mafuta na Serikali imeweza kuokoa pesa nyingi ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya kununua mafuta katika maeneo hayo.

Pia, Serikali imeweza kuondoa

mitambo mikubwa ya IPTL (megawati 103), Aggreko (megawati 48) na Symbion (megawati 120-129) ambapo tumeokoa takribani shilingi bilioni 138. Tulipoondo mitambo hiyo, tuliweza kuokoa kwa mwezi shilingi bilioni 6.9 zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya uendeshaji wake.

Vilevile, Serikali imeweza kuunganisha maeneo mbalimbali katika gridi ya Taifa na kuokoa shilingi bilioni 121. Maeneo hayo ni Tunduru, Mnazimoja mkoani Lindi kuelekeea Luangwa, umbali wa takribani kilomita 80 (kilovoti 132), Liwale, Masasi na Nanyumbu.

Nao, Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydropower Project (JNHP) wa megawati 2,115 unandelea ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85 kulingana na mpango kazi uliopangwa, mradi huo ambao umeajiri jumla ya wafanyakazi 3,897 tangu kuanza utekelezaji wake ambapo kati yao watananza ni 3,422 sawa asilimia 87.81 hadi kukamilika kwa mradi, watananza 6,000 watajiriwa.

Pia, Serikali imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo wa megawati 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 61.

Mwaka 2015, transfoma zilizokuwa zimefungwa nchini kote zilikuwa 12,000.2 lakini leo hii, jumla ya transfoma 23,000.56 zimefungwa nchini sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 100) Pia, Serikali imeendelea na ukarabati wa transfoma zilizokuwa mbovu.

Mwaka 2015, kulikuwa na ngizo za umeme zilizojengwa nchini milioni 1.1. kwa sasa, kuna zaidi ya ngizo milioni 3.7 zilizotumika, hivyo Serikali imeweza usambazaji umeme katika maeneo mengi hivyo kuimarisha kabisa hali ya upatikanaji wa umeme nchini.

Mwaka 2017 kuliwekwa mkakati na kiserikali kuhakikisha kwamba shughuli zote za usambazaji na ujenzi wa kupeleka umeme kwa wananchi, zinafanya kwa haraka. Njia pekee ilikuwa ni kuhakikisha vifaa vinapatikana ndani ya nchi hivyo Serikali ilisitisha rasmi uagizaji vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Wakati huo nchini kulikuwa na kiwanda kimoja cha kuzalisha transfoma, sasa viko vinne. Uwezo wetu wa ndani ulikuwa ni wa uzalishaji transfoma 97, leo hii tuna uwezo wa kuazalisha transfoma 21,000

ingawa mahitaji yetu ni 14,000 kwa sasa. Kwahiylo transfoma zilizopo ni nyingi hadi zinabaki ziada.

Pia, mwaka 2017 Serikali ilisitisha uagizaji wa ngizo kutoka nje ya nchi. Wakati huo, mahitaji yetu ya ngizo yalikuwa milioni 1.2 na uwezo wetu wa ndani ulikuwa 800,000 hivyo zilikuwa hazitoshi. Leo, tuna viwanda 10 ambavyo vinazalisha ngizo zaidi ya milioni 2.5 wakati mahitaji yetu ni chini ya milioni 2 kwa mwaka.

Hii imesaidia sana kutengeneza ajira kwa watananza. Zaidi ya watananza 3,000 wameajiriwa kutokana na uwepo wa viwanda hivi vipyta. Aidha, tumeokoa shilingi bilioni 162.23 kwa kutumia ngizo za ndani ya nchi.

Kwa upande wa mita za LUKU, awali hatukuwa na viwanda hapa nchini. Mwaka 2017 uagizwaji wa mita kutoka nje yan chi ulisitishwa rasmi. Kwa sasa tuna viwanda vikubwa vitatu vya kuzalisha mita za LUKU. Mahitaji yetu ni mita milioni 1.56 wakati uwezo wa kuzalisha ni zaidi ya mita milioni 2.5.

Aidha, tulikuwa na kiwanda kimoja cha nyaya za umeme. Leo tunavyo zaidi ya vinne. Mahitaji yetu ni kilomita 149,000 kwa mwaka watati uwezo wa kuzalisha ni kilomita 250,000.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa linapata hasara wakati ule kiasi cha shilingi milioni 439 lakini leo shirika halina hasara na linatengeneza faida. Kwa mwaka huu wa fedha, shirika limelipa gawio kwa serikali kiasi cha shilingi bilioni 1.43.

Katika hatua nyengine, Usambazaji umeme vijiji umeenda kwa kasi kubwa sana. Mwaka 2010, vijiji viliviyokuwa na umeme ni 562, mwaka 2015 vijiji 2,018, lakini hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya vijiji 9,112 vimeunganishiwa umeme ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 351.54 na Ifikapo Juni 31, 2021 hakutakuwa na kijiji ambacho hakijafikiwa na umeme.

Aidha, mwaka 2015 hatukuwa na Wilaya iliyo kamilika kuunganishiwa umeme katika vijiji vyake vyote. Leo hii zipo jumla ya Wilaya 34 nchini ambazo vijiji vyake vyote vimepata umeme.

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2016 hadi Machi 2020, jumla ya Taasisi 11,164 zimeunganishiwa umeme ikilinganishiwa na Taasisi 4,036 zilizokuwa zimeunganishiwa kufikia Desemba, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 184.88 ambalo ongezeko hilo linafanya jumla ya Taasisi zilizounganishiwa umeme kufikia 15,200.

Kwa nchi za Afrika Mashariki na kwa Afrika kiujuu, Tanzania inaongoza kwa kupeleka umeme vijiji kujliko nchi nyingine.